

Contents

Utangulizi	2
Kujiunga na Umoja na Kiingilio.....	2
Ada ya Kila Mwezi.....	3
Michango mingine.....	4
Taarifa za wanachama.....	4
Ada ya shule	5
Misiba	5
Kutoa Pole.....	7
Ugonjwa	8
Huduma za kiimani na Ndoa.....	10
Mkono wa kwa heri	10
Uthibitisho wa Huduma.....	10
Mikopo.....	11
Kanono Day	12
Mikutano, Vikao na Gharama za mikutano	14
Kanuni za Fedha	15
Ukaguzi wa Hesabu za Umoja (Katiba 6.1.1.8).....	16
Mfuko wa Umoja (Katiba 6.1.).....	17
Usimamizi wa Uwekezaji wa Umoja Kanono Saccos.....	18
Ukodishaji wa Shamba la kanono group (Katiba 6.1.1[k])	19
Faini na Adhabu Mbalimbali.....	19
Taarifa ya madeni ya Wanaumoja	20
Upigaji kura Mkutano Mkuu (Katiba 2.1.13)	21
Utaratibu wa kumfukuza mwanammoja	21
Uchaguzi kwenye Umoja.....	22
Marekebisho ya Kanuni	25
Kupitisha na Kuanza kutumika kwa Kanuni	26

Utangulizi

Kwa vile katiba ni sheria mama ambayo hutoa kwa ujumla miongozo na taratibu za uendeshaji wa taasisi husika, usimamizi wa kina wa shughuli za taasisi huundiwa kanuni ili kuifanya katiba iwe ndogo na utekelezaji wake uwe rahisi kwa malengo ya kueleweka.

Sisi wajumbe wa Halmashauri kwa mamlaka tuliropewa na katiba ya Kanono Group toleo la 2016 Ibara ya 7.2.8(g) baada ya majadiliano tumeamua kutengeneza Kanuni za Umoja ambazo zitawezesha utekelezaji bora wa Katiba kwa mstakabali wa umoja wetu.

Kanuni hizi zitatajwa kama Kanuni za Kanono Group Toleo la 2018 na zitaanza kutumika tarehe 01 Julai, 2018.

Kujiunga na Umoja na Kiingilio

- 1.1. Bila kuathiri masharti ya kifungu cha 4.4.1 cha Katiba ya Umoja, mtu yeyote mwenye asili ya wilaya za Karagwe na Kyerwa atakayependa kujiunga na Umoja atajaza fomu ya maombi ya kujiunga ambayo itajulikana kama K.F.1 na kulipa angalau 50% ya kiingilio kabla ya kuikabidhi kwa katibu wa kanda ambaye ataiwasilisha kwenye kikao cha Viongozi wa kanda kwa ajili ya kujadiliwa. (Katiba 4.4.1(a-e))
- 1.2. Baada ya kuweka maoni yake, Kanda itawasilisha fomu kwa Kamati Kuu ambayo ndiyo itakayokuwa na uamuzi wa mwisho wa kumpokea mwanaumoja mpya (Katiba 4.4.1(f))
- 1.3. Isipokuwa kwa mtu ambaye maombi yake yamekataliwa kwa sababu ya kukosa vigezo vilivyowekwa na kifungu cha 4.2 cha Katiba ya Umoja, kiingilio hakitarudishwa,
- 1.4. Kiingilio kwa mwanachama anayejiunga na umoja kitakuwa shilingi za kitanzania Laki Tatu (Tsh 300,000/-) Tu.
- 1.5. Kiingilio kinaweza kulipwa kwa mkupuo au kwa mafungu lakini kwa vyovyote vile Mwanaumoja awe amemaliza kulipa kiingilio ndani ya miezi minne tangu tarehe ya stakabadhi ya sehemu ya kwanza ya kiingilio vinginevyo itachukuliwa kwamba hajawahi kujiunga na Umoja.

- 1.6. Iwapo itabainika mwanachama aliyejiunga na umoja alitoa taarifa za uongo kuhusu asili yake au taarifa nyingine kwenye fomu ya kujiunga basi uanachama wake utakuwa batili.
- 1.7. Bila kuathiri kifungu cha 4.3 (b) na (c) cha Katiba ya Umoja, Mwanachama aliyejiunga na Umoja ataanza kupata huduma za umoja baada ya miezi sita tangu ajiunge na umoja.
- 1.8. Kamati Kuu haitapokea na/au kujadili fomu ya maombi ya kujiunga na Umoja ya mtu anayetaka kujiunga na Umoja kwa masharti yaliyoainishwa kwenye kifungu cha 4.3 cha Katiba ya Umoja mpaka awe amelipa:
 - (a) ada yote aliyokuwa anadaiwa kabla ya kufukuzwa au kujiondoa kwenye Umoja;
 - (b) adhabu zote alizokuwa anadaiwa kabla ya kufukuzwa au kujiondoa kwenye Umoja ;
 - (c) harambee aliyokuwa anadaiwa kabla ya kufukuzwa au kujiondoa kwenye Umoja; na
 - (d) michango mingine ambayo kabla ya kufukuzwa au kujiondoa kwenye Umoja ilikuwa imepitishwa na kuwa deni kwa wanaumoja.
- 1.9. Mwanachama mpya ataanza kulipa ada ya kila mwezi kuanzia mwezi ambao stakabadhi ya fungu la kwanza la fedha ya kiingilio ilipoandikwa.
- 1.10. Watoto wa Wanaumoja wanaweza kujiunga na Umoja hata kama wanaishi nje ya Mkoa wa Arusha ikichukuliwa kwamba nyumbani kwao ni Arusha kwa wazazi wao

Ada ya Kila Mwezi

- 2.1 Ada ya mwanachama ya kila mwezi itakuwa shilingi Elfu Kumi na Tano (Tshs 15,000/-) Tu. Ada hii inaweza kulipwa kwa mafungu au kwa mkupuo.
- 2.2 Mwanaumoja hatapewa huduma yoyote kati ya huduma zinazotolewa na Umoja iwapo atakuwa hajalipa kikamilifu ada ya kila mwezi kwa muda wa miezi mitatu au zaidi.

- 2.3 Kila Kanda itatoza ada ya kila mwezi kulingana na masharti ya vifungu vya 6.1.2(a) na 10.1.5(j) vya Katiba ya Umoja.
- 2.4 Mweka Hazina wa Kanda atawajibika kuandaa taarifa ya madeni, mapato na matumizi kila mwezi na kuiwasilisha kwa Mweka Hazina wa Umoja (Katiba 7.9.19[c])
- 2.5 Orodha ya wanachama wanaodaiwa miezi mitatu na kuendelea itasomwa mbele ya mkutano mkuu wa umoja na Mwekahazina wa Umoja.
- 2.6 Mwekahazina wa Kanda atasoma taarifa iliyotajwa kwenye kanuni hii kanuni ndogo ya 5 kwenye vikao vyote vya Kanda.
- 2.7 Iwapo kwenye Kanda kuna wanaumoja waliotajwa kwenye kanuni hii kanuni ndogo ya 5 viongozi wa kanda wataweka agenda ya kuwajadili na kuandika kwenye muhtasari hitimisho la mjadala.

Michango mingine

- 3.1 Kwa ridhaa ya mkutano mkuu, na kwa mjibu wa taratibu zilizowekwa na katiba ya umoja, kunaweza kufanyika michango mingine.
- 3.2 Harambee inayohusisha wanaumoja na wageni waalikwa itaitishwa kwa ajili ya kuchangia fedha zitakazowezesha kutekeleza jambo lililokubaliwa na Mkutano Mkuu.
- 3.3 Endapo itafikia kiwango kilichopo kwenye mfuko wa umoja ni pungufu ya Shilingi Million Ishirini (Tsh. 20,000,000/-) na mapato tarajiwa ndani ya miezi sita inayofuata hayawezi kurudisha kiasi kinachopungua, Kamati Kuu itagawa kiasi kinachopungua kwenye mfuko kutoa mapato tarajiwa ya miezi sita ya mbele ili wanaumoja wachangie kiasi kinachobaki ndani ya miezi sita.

Taarifa za wanachama

- 4.1 Kamati kuu itatunza rejista ya taarifa zote za wanachama na wategemezi kwenye daftari maalumu au kwenye mfumo laini wa kompyuta wa Umoja.
- 4.2 Ni jukumu la mwanachama kujaza fomu ya taarifa zake na ndugu zake wanaotambuliwa kikatiba kwa usahihi.

- 4.3 Hakuna mtegemezi wa Mwanaumoja anayetambuliwa kikatiba atahudumiwa na Umoja iwapo hayumo kwenye rejista ya Wanachama (Katiba 3.7.10)
- 4.4 Isipokuwa kwa huduma iliyotajwa na kanuni ya 7 kanuni ndogo ya 4, Mwanaumoja hataomba huduma baada ya miezi mitatu kupita tangu kustahili huduma hiyo.

Ada ya shule

- 5.1 Ada ya shule itatolewa kwa mjibu wa ibara ya 3.2.1 ya katiba ya Umoja.

Misiba

- 6.1 Mara Msiba utokeapo Kamati kuu ya umoja itashirikiana na mfiwa kupanga taratibu zote za msiba kulingana na mazingira ya msiba husika. Hii ni pamoja na maandalizi ya awali ya mazishi na kuhudumia msiba kabla ya kusafirisha mwili wa marehemu.
- 6.2 Mwenyekiti au kiongozi mwingine aliyemteua kumwakilisha atakuwa sehemu ya Kamati ya Msiba na atashiriki kikamilifu kulingana na mazingira ya kila msiba.
- 6.3 Panapotokea msiba, kanda husika ambapo msiba umetokea, italazimika kulala msibani angalau kwa siku moja au mbili kulingana na mazingira ya kila msiba (Katiba 7.5.25[j])
- 6.4 Kusafirisha msiba/mwili wa marehemu nje ya mikoa mitatu kutoka eneo la umauti, Umoja utatoa shilingi za kitanzania Milioni Tatu (Tshs.3,000,000/-) Tu (Katiba 3.2.4)
- 6.5 Kusafirisha msiba/mwili wa marehemu ndani ya mikoa mitatu kutoka eneo la umauti, Umoja utatoa Shilingi za kitanzania Milioni Moja na Laki Mbili (Tsh.1,200,000/-) Tu (Katiba 3.2.4)
- 6.6 Njia ya kusafirisha msiba/marehemu itapangwa na mfiwa kwa kushirikiana na Kamati Kuu. Iwapo kuna njia zaidi ya moja njia fupi itachaguliwa baada ya kuzingatia hali ya kila moja.

- 6.7 Wanaumoja wenye nia ya kusindikiza msiba watajiandikisha kwa kiongozi mwenye dhamana ya mawasiliano kwenye Umoja ndani ya muda utakaokuwa umetangazwa;
- 6.8 Iwapo waliojiandikisha ni wengi kuliko uwezo wa gari lililoandaliwa, Wanaumoja wa Kanda yake watapewa kipaumbele kwanza, wanaotokea kijiji au kata msiba unapopelekwa na baadaye waliojiandikisha wa kwanza;
- 6.9 Kamati Kuu itamteua mmoja wa Wanaumoja wanaosindikiza msiba kuwa kiongozi na mratibu wa wanaumoja wawapo safarini na msibani
- 6.10 Isipokuwa usafiri wa kwenda na kutoka msibani, wanaumoja wanaosindikiza msiba watajitegemea kwa gharama zote;
- 6.11 Gari litakalokodishwa na Umoja kupeleka msiba sehemu ya mazishi litalala msibani siku ya kuzika, litashinda na kulala siku inayofuata na kuondoka alfajiri;
- 6.12 Kulingana na mazingira ya kila msiba, wanaumoja wanaweza kufupisha au kurefusha muda wa ushiriki wao kwenye msiba bila kuongeza gharama wanazoweza kudai kutoka kweye Umoja
- 6.13 Mwanaumoja ambaye ataamua kwenda tofauti na ratiba ya gari lililosafirisha msiba atakuwa huru na atafanya hivyo kwa gharama zake;
- 6.14 Wanaumoja wanashauriwa kuwa na ushiriki mzuri kwenye msiba kuliko kutumia muda wao mwingi kwenye ratiba zisizohusiana na msiba waliosindikiza;
- 6.15 Kwa msiba unaosafirishwa na usiosafirishwa kiasi cha Shilingi Laki Tano (Tsh.500,000) Tu kitatolewa na Umoja kwa ajili ya maandalizi ya awali ya mazishi ((Katiba 3.3.3);
- 6.16 Huduma inayotolewa kwa mujibu wa kanuni hii kanuni ndogo ya15 ni moja kwa msiba bila kujali idadi ya ndugu wenye uhusiano wa kuhudumiwa na Umoja kwa mujibu wa katiba.
- 6.17 Kiasi cha Shilingi Laki Tatu (Tsh.300,000) Tu kitatolewa kwa Kamati ya Huduma za Jamii kwa ajili ya kuhudumia msiba mara tu baada ya tangazo la kifo kutolewa na uongozi wa Umoja (Katiba 3.3.1)

- 6.18 Kiasi chochote cha fedha au vitu kilichobaki kwenye kuhudumia msiba au kutoa pole, baada ya Kamati ya Huduma za Jamii kumaliza kazi ya kutoa huduma, kitakabidhiwa kwa mwanaumoj mfiwa au ndugu zake wa karibu iwapo mwanaumoj ndiye aliyefikwa na umauti. (Katiba 3.3.2)
- 6.19 Iwapo mwanachama atasafiri kwenda sehemu yoyote kwa ajili ya mazishi ya mtegemezi anayetambuliwa na kuhudumiwa kwa mujibu wa katiba atapewa na Umoja nauli kiasi cha Tsh 500,000/- (Katiba 3.2.9)
- 6.20 Bila kuathiri masharti ya kanuni hii kanuni ndogo ya 16, iwapo mwanachama atasafiri kwenda mkoa wowote au ndani ya mkoa wa Arusha kwa ajili ya msiba wa mtegemezi wake anayetambuliwa na katiba atapewa Tshs 500,000/- kwa ajili ya maandalizi ya mazishi. (Katiba 3.3.3)
- 6.21** Iwapo kutatokea janga la kusababisha misiba zaidi ya miwili kwa wakati mmoja na iwapo misiba hiyo inasafirishwa kwenda eneo moja, misiba hiyo inaweza kutolewa huduma ya kusafirisha kwa namna ambayo itapunguza gharama kwa Umoja.

Kutoa Pole

- 7.1 Utaratibu wa Umoja kwenda kwa mfiwa kutoa pole unahusu misiba ambayo itatokea nje ya mkoa wa Arusha, au kama ni ndani ya mkoa wa Arusha iwe wanaumoj hawakuweza kushiriki kwa sababu ya umbali au sababu nyinginezo. (Katiba 3.2.9)
- 7.2 Kamati ya Huduma za Jamii itapewa shilingi za kitanzania Laki Nne (Tsh 400,000/-) Tu kwa ajili ya chakula na vinywaji baridi kwa wanaumoj watakaoenda kutoa pole kwa mujibu wa kanuni hii kanuni ndogo ya 1
- 7.3 Endapo msiba unawahusu zaidi ya mwanaumoj mmoja, shughuli za msiba au kutoa pole zitafanyika kwa pamoja nyumbani kwa mmoja wa Wanaumoj ndugu wa wafiwa ambaye wenyewe watakubaliana.
- 7.4 Iwapo ndugu hawatakubaliana kwa mujibu wa kanuni hii kanuni ndogo ya 3 kwa zaidi ya muda wa miezi sita tangu msiba kutokea huduma ya kutoa pole itafutwa.

- 7.5 Isipokuwa wakikubaliana vinginevyo, iwapo tukio la kutoa pole linawagusa Wanaumoja zaidi ya mmoja, kiasi cha mkono wa pole kitakachopatikana kitagawanywa sawa kwa wanaumoja hao.
- 7.6 Kamati kuu italipa Shilingi Elfu Sabini na Tano (Tsh.75,000/-) Tu kwa mfiwa kwa ajili ya kukodi viti siku ya shughuli ya kutoa pole kwa mfiwa au wafiwa
- 7.7 Wakati wa kutoa pole, kila mwanaumoja atampa mfiwa mkono wa pole wenye kiasi cha fedha kisichopungua Elfu Tatu (Tsh.3, 000) Tu kwa kufuata utaratibu utakaokuwa umewekwa na uongozi. (Katiba 3.3.4)
- 7.8 Wanaumoja wenye udhuru wa kudumu na iwapo wamefiwa na wategemezi wanaotambuliwa na katiba au wenyewe wamefikwa na mauti, watapewa mkono wa pole. (Katiba 3.3.6)
- 7.9 Iwapo kamati kuu itapokea taarifa ya kufa au kufiwa mwanachama anayeishi nje ya mkoa au ndani ya mkoa lakini sehemu ya mbali, italazimika kuwataarifu wanachama wote kuchangia mkono wa pole “akamwani” kupitia kwa viongozi wa Kanda watakoziwasilisha kwa Mwekahazina.
- 7.10 Mwekahazina baada ya kupokea “Akamwani” kutoka kwa viongozi wa kanda atamkabidhi mwakilishi wa mfiwa au mfiwa kwa utaratibu utakao kubaliwa kati ya Mwekahazina na mfiwa. Zoezi hili lazima likamilike ndani ya mwezi mmoja kuanzia tarehe ya kifo.
- 7.11 Wanaumoja watachukuliwa hawakushiriki msiba kwa mujibu wa kanuni hii kanuni ndogo ya 1 iwapo nusu ya Wanaumoja hawakushiriki.

Ugonjwa

- 8.1 Kwa ugonjwa wa kulazwa hospitalini Mwanaumoja au mtegemezi atapewa shilingi Laki Moja (Tsh 100,000/-) Tu kama huduma ya matibabu. (Katiba 3.2.2)
- 8.2 Huduma ya matibabu itatolewa iwapo mnufaika wa huduma za umoja kikatiba atakuwa amelazwa hospitalini siku tatu au zaidi.
- 8.3 Mnufaika wa huduma ya matibabu kikatiba atapewa shilingi laki moja (Tsh 100,000/-) hata kama hakulazwa hospitalini lakini kwa sababu ya aina au

- namna alivyougua ugonjwa umepelekea kuugulia nyumbani kwa zaidi ya mwezi bila kupona na kurejea maisha yake ya kawaida. (Katiba 3.2.3)
- 8.4 Mnufaika aliyetajwa katika kanuni hii kanuni ndogo ya 3 atatakiwa kuthibitisha ugonjwa huo kwa ripoti ya daktari au mwenendo wa matibabu ya hospitali. (Katiba 3.5.1[c])
- 8.5 Huduma ya matibabu inaweza kutolewa tena kwa mnufaika yuleyule kwa mujibu wa kanuni hii kanuni ndogo ya 1 na 3 baada ya miezi sita tangu huduma ileile kutolewa.
- 8.6 Mwanaumoja atatakiwa kutoa taarifa kwa kiongozi mwenye dhamana ya mawasiliano ndani ya masaa kumi na mawili (12) tangu alazwe hospitali ili Wanaumoja wamtembelee kumjulia hali na analazimika kutoa taarifa mara baada ya kuruhusiwa kutoka hospitali.
- 8.7 Mwanaumoja mgonjwa ambaye kwa sababu ya ugonjwa anaougua amepoteza matumaini ya kupona na kuamua kusafiri ili aendelee kuugulia nyumbani, na hivyo kulazimika kusitisha uanachama wake kwenye umoja, atalipwa Shilingi Milioni Moja (Tsh.1, 000,000/-) Tu. (Katiba 3.2.11)
- 8.8 Mwanaumoja ambaye ametajwa katika kanuni hii kanuni ndogo ya 7 atawasilisha barua ya maombi kwenye Kamati Kuu ili alipwe hela ya kwenda kuugua na kwa kufanya hivyo ajue anahitimisha uanachama wake tangu siku ya kulipwa fedha kwa mujibu wa kanuni hii kanuni ndogo ya 7.
- 8.9 Iwapo mgonjwa mnufaika wa huduma iliyotolewa chini ya kanuni hii kanuni ndogo ya 7 akipona na kurudi Arusha atalazimika kufuata taratibu za kujiunga na umoja kwa mujibu wa masharti ya kifungu cha 4.4.1(a) – (f)
- 8.10 Huduma haitatolewa kwa mujibu wa kanuni hii kanuni ndogo ya 7 iwapo hakuna makubaliano kati ya mume na mke ambao kwa pamoja ni mwanaumoja mnufaika wa huduma inayotolewa kwa mujibu wa kanuni hii kanuni ndogo ya 7.
- 8.11 Huduma haitatolewa kwa mujibu wa kanuni hii kanuni ndogo ya 7, iwapo Kamati Kuu itajiridhisha kwamba kwa jinsi anavyougua, hajafikia hatua ya kukata tamaa.

8.12 Bila kujali kanuni hii kanuni ndogo ya 11, Kamati Kuu italazimika kutoa huduma kwa mujibu wa kanuni hii kanuni ndogo ya 7 iwapo mnufaika amewasilisha taarifa ya Daktari wa Hospitali ya Wilaya au Mkoa kuthibitisha kwamba mwanachama huyo yupo kwenye matibabu endelevu (palliative care) ya hatua za mwisho wa maisha.

8.13 Huduma itatolewa kwa mwanaumojia chini ya kanuni hii kanuni ndogo ya 7 endapo amedumu kwenye Umoja kwa muda wa miaka minne au zaidi mfululizo.

Huduma za kiimani na Ndoa

9.1 Mwanaumojia atalipwa na Umoja kiasi cha shilingi Elfu Hamsini (Tshs 50,000/-) Tu iwapo mtegemezi wake atapata ubarikio, kipaimara au tukio jingine la kiimani ambalo linatambuliwa kwa mujibu wa imani ya dini yake. (Katiba 3.2.6)

9.2 Mwanaumojia anayeoa au kuolewa atalipwa shilingi Laki Mbili (Tsh.200, 000/-) Tu. (Katiba 3.2.7)

9.3 Mwanaumojia anayeozza au kuoza atalipwa kiasi cha shilingi Laki Moja (Tsh 100,000/-) Tu. (Katiba 3.2.8)

Mkono wa kwa heri

10.1 Mwanaumojia hai ambaye amekuwa mwanachama wa Umoja kwa muda wa miaka isiyopungua minne na iwapo atahama Arusha na kuamua kukoma kuwa mwanaumojia atalipwa Shilingi Laki Nne (Tsh 400,000) Tu kama mkono wa kwa heri (Katiba 6.2.2[a])

10.2 Huduma itatolewa chini ya kanuni hii kanuni ndogo ya 14 iwapo kuhama kwa mwanaumojia ni kwa kudumu.

Uthibitisho wa Huduma

11.1 Kwa minajili ya kanuni za fedha, wanachama wote watakaokuwa wamepewa huduma ya mchango wa matibabu, mazishi, na safari au kwa sababu nyingine yoyote; watasaini hati ya malipo mara tu baada ya malipo na baadaye kutoa uthibitisho wa kustahili malipo hayo. (Katiba 3.5.2)

11.2 Kielelezo cha udhibitisho wa kulazwa hospitalini ni fomu ya kuruhusiwa kutoka hospitalini inayoonyesha tarehe ya kulazwa na tarehe ya kuruhusiwa; na

uthibitisho wa msiba ni cheti cha kifo au barua ya afisa mtendaji wa kijiji kuthibitisha kutokea msiba husika. (Katiba 3.5.2)

11.3 Ni jukumu la mwanachama atakaye leta barua ya Afisa Mtendaji wa kijiji kwa mujibu wa kifungu cha 3.5.1(b) cha Katiba kuhakikisha kuwa inakuwa na taarifa zifuatazo:-

- i. Anuani ya posta ya ofisi ya Afisa Mtendaji wa Kijiji
- ii. Majina matatu ya marehemu
- iii. Tarehe na mahali pa maziko
- iv. Majina kamili ya afisa mtendaji wa kijiji
- v. Mhuri , tarehe na sahihi ya Afisa Mtendaji
- vi. Namba ya simu ya Afisa Mtendaji wa Kijiji

11.4 Uthibitisho wowote wa huduma hizi lazima utolewe ndani ya siku 60 tangu kutolewa kwa huduma husika; na mwanachama atakayeshindwa kuwasilisha uthibitisho au kuwasilisha uthibitisho usiokidhi atalazimika kurejesha kiasi cha fedha aliyopewa kama huduma ndani ya siku 15 tangu siku 60 kuisha. (Katiba 3.5.2)

11.5 Udanganyifu wowote katika kupata na kutoa huduma yoyote ya umoja ni kosa kubwa sana na la kumfanya mhusika aliyethibitika kufanya hivyo kufutiwa na kufukuzwa uanachama na kuchukuliwa hatua nyinginezo za kisheria.

Mikopo

12.1 Mikopo siyo huduma, hivyo mkopo unaweza kutolewa au usitolewe kutegemeana na uwezo wa mfuko, mwenendo wa mkopaji wa kurejesha mikopo na uamuzi wa mamlaka inayoidhinisha mikopo.

12.2 Mkopaji atakuwa mwanaumoja hai ambaye atakuwa ametimiza miezi 6 au zaidi tangu kujiunga na umoja. (Katiba 6.2.2[a])

12.3 Taratibu za kuomba mkopo ni mwanachama kujaza nakala tatu za fomu maalumu ya maombi ya mkopo mabaya itajulikana kama K.F 2 (Katiba 6.2.2[b])

- 12.4 Mwombaji wa mkopo lazima adhaminiwe na wanachama/Wanaumoja hai wawili ambao pia wana sifa za kupata mkopo huo na ambao hawana deni lolote la mkopo wa Umoja.
- 12.5 Wadhamini watasaini maelezo ya wajibu wao na kuahidi kuyatekeleza kama K.F 2 itakavyo eleza.
- 12.6 Kamati kuu ndiyo mamlaka ya mwisho ya kupitisha au kutopitisha mkopo. (Katiba 6.2.2[d])
- 12.7 Mkopo ni lazima ulipwe ndani ya miezi minne na kwa riba ya 10% kwa kipindi chote. (Katiba 6.2.1[c])
- 12.8 Iwapo muda wa miezi minne umeisha na mkopaji hajamalizia kulipa mkopo wake , mkopaji na wadhamini watawajibika kulipa mkopo na adhabu ya 10% ya mkopo pamoja na riba ndani ya siku thelathini baada ya muda wa kawaida kuisha (Katiba 6.2.3[a])
- 12.9 Iwapo mkopaji na wadhamini watashindwa kuulipa mkopo wote pamoja na adhabu ya 10% hata baada ya nyongeza ya siku thelathini mkopaji na wadhamini wake watafungiwa huduma za Umoja ((Katiba 6.2.3[c])
- 12.10 Iwapo mkopaji na wadhamini watashindwa kulipa hata baada ya siku 30 tangu kufungiwa huduma mkopaji na wadhamini wake watafukuzwa uanachama (Katiba 6.2.2[a])
- Kiasi cha juu ambacho mwanachama anaweza kukopeshwa ni shilingi Laki Nne (Tsh 400,000/-) Tu (Katiba 6.2.1)

Kanono Day

- 13.1 Kanono Day ni suala la kikatiba na la haki kwa kila mwanaumoja kushiriki. (Katiba 2.1.17)
- 13.2 Mfuko wa Umoja utachangia kiasi cha fedha kilichoombwa na Kamati ya Maandalizi ya Kanono Day, kukubaliwa na Kamati Kuu ambayo itaomba Mkutano Mkuu au itaruhusu Kamati ya Maandalizi ya Kanono Day kuomba Mkutano Mkuu kuridhia ili kufanikisha maandalizi ya sherehe ya Kanono Day

- 13.3 Sikukuu ya Kanono Day itafanyika kila jumapili ya mwisho wa mwezi Julai kila mwaka.
- 13.4 Bila kuathiri masharti ya kanuni hii kanuni ndogo ya 2, kila familia yenye baba, mama na mtoto mmoja itachangia kiasi cha fedha kitakachotangazwa na Kamati ya Maandalizi ya Kanono Day.
- 13.5 Kila familia ya mwanaumoja itakayozidisha washiriki waliotajwa kwenye kanuni hii kanuni ndogo ya 3 itamgharamia kila mshiriki wa ziada kiasi cha fedha ambacho Kamati ya maandalizi ya Kanono Day itaomba Kamati Kuu na kuridhiwa na Mkutano Mkuu au Wanaumoja waliokusanyika kwenye tukio la kutoa pole.
- 13.6 Kila mwanaumoja analazimika kuthibitisha kwa mwenyekiti wa Kamati ya Maandalizi ya Kanono Day au mjumbe mwingine wa Kamati aliyeteuliwa na Mwenyekiti wa Kamati idadi ya wanafamilia wake watakaohudhuria Kanono Day ndani ya muda utakaotangazwa na Mwenyekiti wa Kamati.
- 13.7 Ili kuweka sawa bajeti ya Kanono Day, Kamati itaandaa bajeti Mwezi Januari na kuiwasilisha kwenye Kikao cha Halmashauri cha Mwezi Februari baada ya kuridhiwa na Kamati Kuu; michango itatangazwa kwa Wanaumoja kwenye Mkutano Mkuu wa Mwezi March baada ya kuridhiwa na Mkutano Mkuu kwa kura zilizo nyingi.
- 13.8 Kamati itaratibu na kusimamia sherehe nzima ya Kanono Day. Kamati hii itahakikisha Kanono Day inakuwa na vionjo mbalimbali na hivyo kuifanya kuwa ya kipekee kwenye familia ya wanaasili ya Karagwe na Kyerwa.
- 13.9 Kwenye Mkutano Mkuu utakaofanyika baada ya sherehe ya Kanono Day wanaumoja watafanya tathmini na kutoa mapendekezo ya kuboresha Kanono Day kwa mwaka unaofuata.
- 13.10 Bila kuathiri masharti ya kifungu cha 7.4.1.2 cha Katiba ya Umoja na kwa maelekezo ya Kamati Kuu, Katibu Mkuu atateua Wanaumoja kwa idadi ifaayo kuwa wajumbe wa Kamati ya Maandalizi ya Kanono Day ili kufanikisha kwa ufanisi mkubwa maandalizi ya sherehe ya Kanono Day.

Mikutano, Vikao na Gharama za mikutano

- 14.1 Isipokuwa kwa vikao vya Kamati Kuu na vile vya kamati za kikatiba ambavyo wajumbe wanaweza kujipangia siku na muda wa vikao kulingana na mazingira ya wajumbe, muda wa kuanza vikao, mikutano au kutoa pole utakuwa ni saa 9:00 alasiri na kumaliza saa 12:00 jioni . (Katiba 2.1.19)
- 14.2 Endapo kutakuwa na ulazima wa mkutano kuendelea baada ya saa 12:00 jioni, Mwenyekiti wa kikao au Mkutano ataomba ridhaa ya kuongeza muda hadi nusu saa na maombi hayo yatafanywa dakika 15 kabla ya muda wa kawaida kuisha. Maombi hayo lazima yakubaliwe na wajumbe walio wengi.
- 14.3 Kutaandaliwa daftari la mahudhurio kila kikao, msiba, kutoa pole na Mkutano Mkuu na Akidi ya Mkutano Mkuu ni asilimia 60% ya wanachama wote watakao kuwa tayari wamejiandikisha kuondoa wenye udhuru wa kudumu. (Katiba 7.1.5)
- 14.4 Mwanachama ambaye atashindwa kuhudhulia Mkutano Mkuu, kutoa pole, kikao cha Kanda au vikao vya viongozi kwa sababu za msingi lazima aombe udhuru saa moja kabla ya kuanza kikao, Mkutano au kutoa pole.
- 14.5 Mwanaumojja atakaye omba udhuru kwa masharti ya kanuni hii kanuni ndogo ya 4 atachukuliwa kuwa maombi yake ya udhuru yamekubaliwa iwapo amepokea majibu ya kukubaliwa na yanayoweza kuthibitika.
- 14.6 Kabla ya Mkutano au kutoa pole, kikao cha Kanda au kikao cha viongozi kuanza Mwenyekiti atamwagiza Katibu Mkuu kusoma majina ya walioomba udhuru.
- 14.7 Ni mwanachama wa umoja au mwenza wa ndoa wa mwanachama pekee mwenye wajibu wa kuhudhuria na haki ya kupiga kura katika mkutano au kikao. (Katiba 2.1.13)
- 14.8 Mwanaumojja ambaye atakuwa mwenyeji wa mkutano mkuu atapewa Shilingi Efu Sabini na Tano (75,000/-) Tu kwa ajili ya ukodishaji wa viti na Shilling Laki Moja (100,000/-) kwa ajili ya soda na maji. (Katiba 7.1.12)

- 14.9 Umoja utalipa Shilingi Eelfu Tano (Tsh 5,000) Tu kwa kila mjumbe anayehudhulia vikao vya Halmashauri, Kamati Kuu, na Kamati za Kikatiba kwa ajili ya soda au maji. (Katiba 6.1.1.10[b])
- 14.10 Umoja utatoa Shilingi Eelfu Ishirini (Tsh. 20,000) kila mwezi kwa kiongozi aliyepewa dhamana ya mawasiliano kwa ajili ya mawasiliano.(Katiba 6.1.1.10[b])
- 14.11 Mweka hazina atapewa Shilingi Laki Mbili (Tsh200,000/-) Tu kwa ajili ya matumizi madogomadogo (petty cash) kila mwezi na iwapo haitatumika au kusalia lazima usuluhisho (reconciliation) kati ya mwezi ulioisha na unaoanza ifanyike ili kuondoa usumbufu wa kurudisha salio la matumizi madogomadogo (petty cash) benki. (Katiba 6.1.1.10[b])
- 14.12 Miezi ambayo Mkutano Mkuu unafanyika au miezi ambayo kutakuwepo na vikao vya Kamati mbalimbali au baraza la Wazee, kiasi cha matumizi madogomadogo (Petty Cash) inaweza kuongezwa hadi Tshs 300,000/- kwa mwezi.

Kanuni za Fedha

- 15.1 Kutakuwa na kitabu cha mali za umoja kitakachotunzwa na Mweka Hazina wa Umoja. (Katiba 10.1.5 [a])
- 15.2 Vitabu vyote vya stakabadhi, hati za malipo na mali zote vitasajiliwa kwa namba maalumu katika kitabu cha mali cha Umoja.
- 15.3 Baada ya uongozi kumaliza muda wake, Mwekahazina atakabidhi kitabu cha mali kwa uongozi mpya.
- 15.4 Kila malipo yote yanayofanywa na Umoja lazima yathibitishwe kama kanuni za malipo zinavyotaka. Kukosa uthibitisho kutoka kwa kiongozi au mwanaumoja juu ya matumizi ya fedha yoyote atabeba wajibu wa kurudisha fedha hizo. (Katiba 10.1.5[f])
- 15.5 Makusanyo yote yanayofanyika lazima yalipwe benki na kukatiwa stakabadhi baada ya mlipaji kuwasilisha pay-in-slip halisi kwa mweka hazina. (Katiba 10.1.5[g])

- 15.6 Kwa kutambua unyeti wa shughuli ya harambee na/au mnada inayoendeshwa na Umoja, Mwekahazina anaweza kupokea fedha taslim za malipo yote yanayofanyika kwenye mnada husika na ni lazima azipeleke au asababishe zipelekwe benki ndani ya siku mbili tangu tarehe ya mnada na baadaye kutoa stakabadhi.
- 15.7 Bila ya kuathiri kanuni ndogo ya 6 ya kanuni hii na masharti ya kifungu cha katiba cha 6.1.1.2 ni kosa kwa mwanachama au kiongozi yoyote asiyekuwa na idhini ya Mwekahazina kupokea fedha taslim kwa niaba ya Umoja.
- 15.8 Kila mlipaji ni lazima aandike kwenye Bank Deposit Slip jina lake, na dhumni la malipo hayo mfano faini, adhabu, mkopo, kiingilio, ada ya mwezi, nakadhalika.
- 15.9 Mwanaumoja sharti alipe madeni ambayo muda wake ni mrefu kabla ya kulipa madeni mapya
- 15.10 Malipo yote yanayofanywa na Umoja kwenda kwa mtu yeyote ni lazima yawe na ushahidi wa maandishi aidha kwa stakabadhi iliyotolewa au maandishi mengine kulingana na taratibu za katiba au kanuni hizi.
- 15.11 Malipo yote kuanzia Tsh 100,000/- yatakayofanywa kwa mwanaumoja au mtu mwingine yeyote na umoja yatalipwa kwa kutumia hundi (bank cheque) na malipo yote chini ya Tsh 100,000/- yatalipwa kwa pesa taslimu kutoka kwenye petty cash na kusaini kwenye petty cash voucher.
- 15.12 Bila kuathiri masharti ya kanuni hii kanuni ndogo ya 9, malipo yanayozidi Tshs 100,000/- yanaweza kulipwa Taslim pale mazingira yanapolazimu

Ukaguzi wa Hesabu za Umoja (Katiba 6.1.1.8)

- 16.1 Kamati kuu itateua mkaguzi wa fedha wa nje (external auditor) mwenye sifa zinazotambuliwa na mamlaka za nchi.
- 16.2 Mkaguzi wa fedha wa nje atateuliwa kutoka miongoni mwa wanaumoja na kama hayupo atateliuwa nje ya wanaumoja.
- 16.3 Iwapo mkaguzi wa fedha atatoka ndani ya umoja atalazimika asiwe kiongozi.

- 16.4 Mkaguzi wa fedha atathibitishwa kila baada ya miaka miwili tangu kuteuliwa japo kwa sababu za msingi juu ya utendaji wake Halmshauri inaweza kumwondoa na kuthibitisha mwingine muda wowote.
- 16.5 Halmashauri inaweza kupitisha posho ya Mkaguzi wa Nje ambaye siyo Mwanaumoya kadri itakavyoona inafaa lakini kwa vyovyote vile isiwe zaidi ya Tshs 500,000/-
- 16.6 Majina ya wakaguzi wa nje yaliyoteuliwa na kamati kuu yatachambuliwa na mmojawapo kuthibitishwa na Halmashauri
- 16.7 Iwapo kuna tuhuma za ubadhirifu wa fedha dhidi ya Kamati Kuu, Halmashauri inayo mamlaka na uhuru wa kuteua na kuthibitisha mkaguzi yeyote wa nje ambaye si Mwanachama wa Kanono Group kwa ajili ya kufanya ukaguzi maalum.
- 16.8 Iwapo Mkaguzi wa nje ameteuliwa na kufanya ukaguzi kwa mujibu wa kanuni ndogo ya 7 ya kanuni hii, taarifa ya matokeo ya ukaguzi itakabidhiwa kwenye kikao cha Halmashauri.
- 16.9 Kiongozi yeyote atawajibishwa na mamlaka mbali mbali kutokana na ripoti ya mkaguzi wa nje ikiwemo kulipa gharama ya fedha, kusimamishwa uongozi, na ikibidi baadaye kufukuzwa uanachama.
- 16.10 Ripoti ya ukaguzi wa fedha ni jambo la lazima na lisilo na mjadala. Uongozi utakaoshindwa kuwasilisha ripoti halisi na kuisoma mbele ya mkutano mkuu wa Desemba bila sababu za msingi utawajibishwa na mkutano mkuu.

Mfuko wa Umoja (Katiba 6.1.)

- 17.1 Isipokuwa kwa matukio yasiyoweza kuzuilika, muda wote Mfuko wa Umoja utakuwa na salio lisilopungua Shilingi Milioni Ishirini (Tsh 20,000,000/-) Tu (Katiba 6.1.1.9).
- 17.2 Bila kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya 1 ya kanuni hii, muda wowote ule, Akaunti za Benki zitakuwa na kiasi cha fedha kisichopungua Milioni Tisa (Tshs 9,000,000) Katiba 6.1.1.9 (a)
- 17.3 Iwapo itatokea Mfuko wa Umoja ukawa chini ya TZS 20,000,000/- na kwa vyovyote vile makusanyo yanayotegemewa kwenye kipindi cha miezi sit

inayofuatia hayawezi kuirudisha, Kamati Kuu itagawa sawa kwa wanaumoja wote kiasi kisichoweza kurudishwa ili Wanaumoja wakichange ndani ya miezi sita kwa mujibu wa Kifungu cha 6.1.1(e) cha Katiba ya Umoja.

- 17.4 Ili kupata kiasi cha fedha kinachohitajika kwa mujibu wa kanuni hii kanuni ndogo ya 3, kiasi cha fedha kinachohitajika kitagawanywa sawa kwa Wanaumoja wachange.
- 17.5 Mwanaumoja atakaye shindwa kuchanga mchango wa kutunisha kwa mujibu wa kanuni hii kanuni ndogo ya 3 atasimamishwa kupokea huduma za umoja na hatua nyingine kufuatia kwa mujibu wa kifungu cha 4.7.2(d) cha Katiba ya Umoja.
- 17.6 Mweka hazina na Weka hazina wa kanda na kamati za kikatiba kwa kushirikiana na kamati ya Fedha na Uchumi watabuni namna bora ya ukusanyaji wa mapato ili kuhakikisha mfuko wa umoja unakua kifedha. (Katiba 7.3.7&7.3.5)

Usimamizi wa Uwekezaji wa Umoja Kanono Saccos

- 18.1 Kwa asili ya majukumu yake, Mweka Hazina atakuwa msimamizi wa kila siku wa uwekezaji wa Umoja kwenye Kanono SACCOS na mahali pengine Umoja utakapoamua kuwekeza.
- 18.2 Kwa asili ya majukumu yake, Mwenyekiti ni mwakilishi wa Umoja kwenye mialiko yote ya nje, hivyo yeye au mwanaumoja aliyemteua kumwakilisha atahudhuria Mikutano yote ya SACCOS au sehemu nyingine ambayo Kanono Group ina uwekezaji au maslahi na kusimamia maslahi ya Umoja yanayohusu uwekezaji wake (Katiba 10.1.1[j])
- 18.3 Kazi kubwa ya mwakilishi wa Umoja kwenye Mkutano wa Kanono SACCOS au sehemu nyingine yenye uwekezaji au maslahi ya Umoja ni kupiga kura na kuamua mstakabali wa maslahi ya Umoja kwa niaba ya Wanaumoja wote.
- 18.4 Mwakilishi huyu kwa wadhifa wake atasimama kama Kanono Group mahala ambapo Kanono Group ina uwekezaji au maslahi mengine.
- 18.5 Ijulikane kuwa Mwakilishi wa Kanono Group sehemu Umoja ulipowekeza ni kujitolea kwa maslai mapana ya umoja na atalipwa Tsh 5,000/- tu kutoka kwenye mfuko wa Umoja kwa kila siku atakayowakilisha Umoja kama kifuta

jasho. Mkutano Mkuu unao uhuru wa kumuuliza chochote kuhusu mustakabali wa uwekezaji wa Umoja.

Ukodishaji wa Shamba la kanono group (Katiba 6.1.1[k])

- 19.1 Ukodishwaji wa shamba la Kanono Group utafanyanyika kwa wanachama wa Kanono Group tu
- 19.2 Shamba litakodishwa kwa kila msimu wa kuanzia 1st February Mpaka 30 August kila mwaka kwa tozo ya Tsh 50,000/- kwa shamba zima.
- 19.3 Maombi ya kukodishwa shamba yatakuwa wazi kuanzia September mpaka 31 January mwaka unaofuata.
- 19.4 Kupitia Mkutano Mkuu au njia nyingine ifaayo, Kamati Kuu itawatangazia wanachama wanaohitaji kukodi kiwanja waandike barua za maombi.
- 19.5 Iwapo waombaji ni wengi aliyetangulia kuomba atapewa
- 19.6 Ili kuweka fursa sawa kwa wote, endapo aliyetangulia kuomba kwa mujibu wa kanuni hii kanuni ndogo ya 5 alikuwa mpangaji kwenye kiwanja msimu kabla ya msimu ambao mwanaumoja wameleta maombi atapewa aliyefuata kwa kuwahi
- 19.7 Waombaji wajibiwe ndani ya siku saba kutoka siku ya mwisho ya kupokea maombi
- 19.8 Mwanaumoja aliyepitishwa na Kamati Kuu kukodi shamba/kiwanja atalazimika kulipa kabla ya kuanza shughuli zozote za kilimo;
- 19.9 Iwapo mwanaumoja atashindwa kulipa kulipa kwa masharti ya kanuni hii kanuni ndogo ya 9 atapoteza haki ya kulikodi na litatolewa kwa mwombaji anayefuata kwa vigezo vilivyoainishwa kwenye kanuni hii kanuni ndogo ya 6

Faini na Adhabu Mbalimbali

- 20.1 Muda wote viongozi wa umoja ngazi zote wachukue jukumu la kutoa elimu na kumsaidia mwanaumoja kuelewa kuwa kwa tabia anazoonyesha anavunja katiba na anaenda kinyume na maelekezo ya kanuni za umoja (Katiba 8.3[b])
- 20.2 Mwanaumoja aliyefikishwa mbele ya kamati ya Nidhamu na Maadili na akakutwa na hatia ya kuvunja katiba au kwenda kinyume na kanuni za

umoja ataadhibiwa. Kamati itamwamuru kulipa gharama za umoja zilizotumika wakati wa kushughulikia shauri hilo na kumwamuru kulipa faini ambayo Kamati itaona inafaa baada ya kuzingatia uzito wa makosa na mwenendo wa Mwanaumoja [Katiba 5.4.2(e)]

- 20.3 Kwa minajili ya kupanua wigo wa mapato, faini zote zitakazotozwa kwenye Kanda, Kamati za Kikatiba, Kamati Kuu, Halmshahauri na Mkutano Mkuu au kwa masuala mengine yasiyokuwa na uhusiano na vikao vilivyotajwa zitalipwa kwenye mfuko wa umoja kwa utaratibu wa malipo ya Umoja. (Katiba 6.1.1)
- 20.4 Kiongozi au Mwanaumoja atakayetozwa adhabu ya kutohudhuria au kuchelewa kikao cha Kanda, Kamati ya kikatiba, Kamati Kuu, Halmashauri au Mkutano Mkuu atailipa ndani ya siku 90.
- 20.5 Adhabu ya Kutohudhuria kikao chochote halali cha Umoja, kutoa pole au msiba bila ruhusa kwa mujibu wa katiba ni Tshs 7,000/- (Katiba 5.1.4(b))
- 20.6 Adhabu ya Kuchelewa kwa zaidi ya dakika 15 kwenye mkutano, kikao chochote au kutoa pole ni Tshs 5,000/-.
- 20.7 Adhabu ya makosa yote yaliyoainishwa chini ya kifungu cha 5.1.1 cha katiba ya Umoja ni Tsh.5,000/-
- 20.8 Iwapo ni faini zinatokana na kutotimiza wajibu kwenye Kanda, Mwekahazina wa kanda apeleke majina Kamati Kuu ndani ya siku saba tangu kikao kufanyika. (Katiba 5.1.4[c]-[e])

Taarifa ya madeni ya Wanaumoja

- 21.1 Pamoja na taarifa ya michango ya kila mwezi, kila Mwekahazina wa kanda atawasomea wanaumoja wote kwenye kanda taarifa ya wanaodaiwa madeni mbalimbali ya umoja.
- 21.2 Taarifa ya madeni kwa wanaumoja itatolewa kila mwezi.(Katiba 10.1.5[c])
- 21.3 Ni wajibu wa Kamati kuu kuandaa taarifa ya madeni ya kila kanda ili kila Mwekahazina wa Kanda aichukue na kuisoma kwenye kikao cha Kanda.(Katiba 10.1.12[c-d])

Upigaji kura Mkutano Mkuu (Katiba 2.1.13)

- 22.1 Maamuzi ya Umoja yatakayohitaji kufikiwa kwa kupiga kura, yatatambuliwa kuwa halali kutokana na kura halali tu zitakazopigwa
- 22.2 Kura halali ni kura ambayo itapigwa na mwanaumojasiyeoasiyeo na kuolewa, mke au mme wa mwanaumojasiyeoasiyeo. Itakuwa kinyume cha Katiba ya umoja kwa mgeni au mtegemezi kupiga kura.
- 22.3 Kura zitachukuliwa halali iwapo idadi iliyopigwa ni sawa na wanaumojasiyeoasiyeo na wenza wao wa ndoa waliohudhuria mkutano husika.
- 22.4 Kila mkutano lazima uwe na akidi inayotakiwa na kanuni hizi.

Utaratibu wa kumfukuza mwanammoja

- 23.1 Iwapo Kamati Kuu itaona mwanachama yeyote amekiuka katiba au kanuni hizi na anatakiwa kufukuzwa uanachama itapitisha azimio la lengo la kumfukuza mwanachama katika Umoja. (Katiba 5.2.1)
- 23.2 Azimio ni lazima litaje kosa analotuhumiwa nalo na kwa kiasi gani kosa hilo adhabu pekee ni kufukuzwa uanachama.
- 23.3 Nakala ya Azimio hilo atapewa mwanachama na Katibu wa Kanda.
- 23.4 Baada ya azimio kupitishwa na Kamati Kuu, Katibu Mkuu ataliwasilisha kwenye Kikao cha Halmashauri ambayo itamwalika Mwanachama husika kwa ajili ya kusikiliza utetezi wake.(Katiba 5.2.3)
- 23.5 Nukuu yoyote ya maelezo inayoandikwa na katibu wa Kikao cha Halmashauri wakati wa kusikiliza shauri lazima mhusika asomewe na kama anakubali ndicho alichokitamka atie sahihi yake kila ukurasa wa nukuu hizo.
- 23.6 Halmashauri itapokea nyaraka zote za maandishi na kuziambatisha na nukuu za maelezo ya Mwanaumojasiyeoasiyeo ili kujiridhisha na uzito wa makosa.
- 23.7 Baada ya kumsikiliza, Halmashauri, ikimkuta mwanachama anayetuhumiwa ana hatia inaweza:
 - (a) kutoa masharti ya Mwanaumojasiyeoasiyeo kujirekebisha na kurejea kwenye utaratibu wa Umoja ndani ya muda itakao ona unafaa;
 - (b) Kumuweka chini ya kipindi cha uangalizi

- (c) Kumfukuza kwa mujibu wa kifungu cha 5.2.6 cha Katiba ya Umoja
- 23.8 Bila kuathiri masharti ya kifungu cha 5.3.3 cha Katiba ya Umoja, mwanaumoja asiporidhika na uamuzi wa Halmashauri, ndani ya siku 28 tangu kupokea barua ya kufukuzwa anaweza:
- 23.8.1 Kuwasilisha maombi kwa Halmashauri akiomba irejee uamuzi wake (Katiba 5.3.2);
- 23.8.2 Kukata rufaa Mkutano Mkuu (Katiba 5.3.1)
- 23.9 Baada ya kupokea rufaa kwa mujibu wa kanuni hii kanuni ndogo ya 24.7(b), Katibu Mkuu atalazimika kuiweka kwenye agenda za Mkutano Mkuu wowote utakaoitishwa mapema tangu kupokea maelezo ya mkata rufaa;
- 23.10 Iwapo Mwanaumoja hakutii wito wa kufika mbele ya Halmashauri kujitetea kwa mujibu wa kifungu cha 5.2.3 atawajibika kuueleza na kutoa ushahidi wa kuridhisha mbele ya Mkutano Mkuu kwamba alikuwa na sababu za msingi kwa mujibu wa kifungu cha 7.4.7.2.6 cha Katiba zilizo mfanya ashindwe kutii wito wa kufika mbele ya Halmashauri kusikilizwa.
- 23.11 Iwapo atashindwa kuonyesha kwa ushahidi kwamba sababu zilizotajwa kwenye kifungu cha 7.4.7.2.6 au nyingine zenye uzito sawa na hizo zilimfanya ashindwe kutii wito rufaa yake itatupiliwa mbali.
- 23.12 Iwapo rufaa haitakataliwa kwa mujibu wa kifungu cha 5.3.3 cha Katiba ya Umoja, mwenye kukata rufaa, ili afaulu katika rufaa, sharti kuuridhisha Mkutano Mkuu kwa kuainisha makosa ambayo Halmashauri ilifanya na ambayo kama yasingekuwepo uamuzi wa kumfukuza usingefikiwa.

Uchaguzi kwenye Umoja

- 24.1 Kutakuwepo na Kamati ya Uchaguzi kwa mujibu kifungu cha 7.5 cha Katiba ya Umoja toleo la 2016.
- 24.2 Wajumbe wa Kamati ya uchaguzi ni Wenyeviti wa Kanda zote na Makatibu wa Kanda zote (Katiba 2.1.20)

- 24.3 Kwa muda unaofaa kabla ya Uchaguzi Kamati Kuu itaitisha kikao cha Pamoja kitakachojumuisha Wenyeviti wa Kanda, Makatibu wa Kanda na Kamati ya Wazee ili kuwaweka pamoja kupitia vifungu vya Katiba vinavyohusu uchaguzi.
- 24.4 Kwenye kikao kitakachoitishwa kwa mujibu wa Kanuni hii kanuni ndogo ya 3 Kamati ya Uchaguzi itawachagua Mwenyekiti na Makamu mwenyekiti miongoni mwa Wenyeviti wa Kanda na uchaguzi huu utasimamiwa na Kamati ya Wazee.
- 24.5 Viongozi watakoachaguliwa kwa mujibu wa kanuni hii kanuni ndogo ya 4 watatokana na wenyeviti wa Kanda,
- 24.6 Baada ya uchaguzi wa Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Uchaguzi, Katibu Mkuu atawateua Katibu na Katibu Msaidizi wa Kamati ya Uchaguzi miongoni mwa makatibu wa Kanda. Uteuzi huu utazingatia majina yaliyopitishwa na kikao cha Kamati Kuu kulingana na masharti ya ibara ya 7.8 ya Katiba ya Umoja.
- 24.7 Baada ya Kamati Uchaguzi kupata viongozi kikao cha pamoja kitapitia vifungu vya Katiba na Kanuni ili Kamati ya Uchaguzi itoke na uelewa wa mchakato wa Uchaguzi.
- 24.8 Uchaguzi wa Viongozi wa Umoja utaitishwa kwa mujibu wa masharti ya vifungu vya Katiba vya 9.1.1, 9.1.2 na 9.1.3.
- 24.9 Iwapo uchaguzi utashindikana kufanyika kwa sababu zozote zile baada ya uongozi kujiuzulu kwa mujibu wa kifungu cha 9.1.5 cha katiba ya Umoja, Mwenyekiti wa Kamati ya Uchaguzi, Katibu wa Kamati ya Uchaguzi, wasaidizi wao na Wajumbe wa Kamati ya Uchaguzi wataongoza Umoja mpaka viongozi watakapopatikana.
- 24.10 Uongozi wa Umoja kwa mujibu wa Kanuni hii kanuni ndogo ya 8 utajulikana kama uongozi wa mpito.
- 24.11 Isipokuwa kama nchi ipo kwenye hali ya vita, au mamlaka za nchi zimetangaza hali ya hatali, Uongozi wa mpito utawajibika kuitisha Mkutano Mkuu wa Uchaguzi ndani ya siku 14 tangu Mkutano wa awali kuvunjika.
- 24.12 Uongozi wa mpito hautaruhusiwa kufanya maamuzi ambayo athari zake kwa Umoja au Mwanaumoja zitaendelea kuwepo nje ya kipindi cha uongozi wa mpito;

- 24.13 Isipokuwa kwa huduma zilizoainishwa chini ya vifungu vya 3.2.4, 3.2.9, 3.3.1, 3.3.3 vya Katiba ya Umoja na gharama za vikao au Mkutao Mkuu, uongozi wa mpito hautafanya matumizi au kuidhinisha malipo kwa niaba ya Umoja.
- 24.14 Kwa malengo ya kuhakikisha huduma zinatolewa kwa mujibu wa Kanuni hii kanuni ndogo ya 13, makatibu wa Kanda watakuwa Wajumbe wa Kamati ya Huduma za Jamii ya Uongozi wa Mpito.
- 24.15 Kamati ya huduma za Jamii kwa mujibu wa kanuni hii kanuni ndogo ya 14 itaongozwa na Katibu wa Uongozi wa Mpito kama Mwenyekiti na Katibu wa Kamati atakuwa Katibu wa Uongozi wa Mpito.
- 24.16 Iwapo wajumbe wa Kamati ya Huduma za Jamii ya Mpito hawatoshi kulingana na majukumu yaliyopo, Mwenyekiti na Katibu wa Uongozi wa mpito watateua Wanaumoja wa Kanda ambayo kwenye eneo lake huduma inatolewa ili wawe wajumbe wa Kamati ya Huduma za Jamii ya Uongozi wa Mpito kwa tukio la huduma hiyo tu.
- 24.17 Uongozi wa mpito hautatoa stakabadhi za Umoja kutambua malipo ya ada, adhabu, mnada, kutunisha au michango mingine kutoka kwa Wanaumoja. Kila Mweka Hazina wa Kanda atapokea Bank Deposit Slip na kuzihifadhi ili azikabidhi kwa Mwekahazina baada ya uchaguzi kufanyika.
- 24.18 Bila kujali masharti ya kifungu cha 6.1.1.1(b) & (c), kwenye kipindi cha uongozi wa mpito, Wanaumoja wataendelea kulipa madeni kwa kuweka fedha benki na kukabidhi Bank Deposit Slip kwa Mweka Hazina wa Kanda.
- 24.19 Bila kujali masharti ya kifungu cha 6.1.1.1(c) cha Katiba ya Umoja, kwenye kipindi cha uongozi wa mpito, Mwanamoja akikabidhi Deposit Slip kwa Mwekahazina wa Kanda atahesabika kuwa amelipa.
- 24.20 Mweka Hazina wa Kanda ataandika upande wa nyuma wa Deposit Slip tarehe ya kuipokea na atasaini.
- 24.21 Iwapo ni lazima kuna uhitaji wa fedha, uongozi wa mpito lazima upitishie matumizi hayo kwa asilimia 80 ya Wajumbe wote.

Marekebisho ya Kanuni

- 25.1 Kanuni hizi zipitishwe na kura zaidi ya asilimia 75% ya wajumbe wote wa Halmashauri.
- 25.2 Halmashauri inaweza kubadilisha na/au kurekebisha, kanuni hizi muda wowote iwapo itaona kuna umuhimu wa kufanya hivyo. Mabadiliko yoyote ya kanuni hizi kwa mujibu wa kanuni hii yatafanyika baada ya kupata kura 75% au zaidi ya wajumbe wote wa Halmashauri.
- 25.3 Katika kujadili kanuni Halmashauri itapiga kura kupitisha kanuni moja baada ya nyingine. Asilimia 51 ya kura za wajumbe waliohudhuria kikao zitapitisha Kanuni moja moja
- 25.4 Iwapo kura zinazohitajika kuamua kupitisha marekebisho kwenye kanuni hizi baada ya kupitisha kanuni moja moja hazitapatikana kwenye upigaji kura wa kwanza kwa mujibu wa kanuni hii kanuni ndogo ya 1, Wajumbe wa Halmashauri watarudia kupiga kura hadi mara tatu.
- 25.5 Kura zisipotosha baada ya kupiga kura mara ya tatu, Mwenyekiti atatoa rai ya kuahirisha kikao mpaka siku nyingine ya karibu ambayo kikao kingine kitaitishwa.
- 25.6 Iwapo kwenye kikao kilichoitishwa kwa mujibu wa kanuni hii kanuni ndogo ya 5 kura zitapigwa na 75% ya kura zisipatikane baada ya kupiga kura mara tatu, kura zitapigwa mara ya nne ambapo Kanuni zitapitishwa kwa asilimia 60 ya kura zote.
- 25.7 Iwapo asilimia 60 ya kura zote haitapatikana kupitisha mabadiliko ya Kanuni hizi kwa mujibu wa kanuni hii kanuni ndogo ya 6, Halmashauri itarejea kwenye kanuni zilizosababisha kanuni kukataliwa na vitarekebisha kulingana na maoni ya walio wengi ilimradi marekebisho hayo hayalengi kutunga kanuni zinazopingana na Katiba.

Kupitisha na Kuanza kutumika kwa Kanuni

Kanuni hizi zimepitishwa na asilimia 82 ya wajumbe wa Kikao cha Halmshahuri siku ya 26 ya mwezi wa Aprili, mwaka 2018 katika ukumbi wa Hoteli ya City Link na kusainiwa na katibu na mwenyekiti wa Umoja ili zianze kutumika kuanzia tarehe 01 Julai, 2018.

Jina la Katibu.....

Sahihi.....

Jina la Mwenyekiti.....

Sahihi.....